# LEARNING BY EAR

# ”If a tree falls… - Deforestation in Africa"

## EPISODE THREE: "Women have their say"

**AUTHOR: Romie Singh**

**EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz**

**PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis**

## List of characters EPISODE THREE:

**Narrator**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **SCENE 1** | **Mother (f, 36)** | | |
| **SCENE2** | **Chika (f, 18)** | **Mother (f, 36)** | |
| **SCENE 3** | **Akiki (f, 7)** | **Isi (m, 18)** | |
| **SCENE 4** | **Chief (m, 40)** | **Talib (m, 20)** | |
| **SCENE 5** | **Mulogo (m, 22)** | **Chika (f, 18)** | |
| **SCENE 6** | **Mother (f, 36)** | **Chika (f, 18)** | **Group of Women** |
| **SCENE 7** | **Isi (m, 18)** | **Akiki (f, 7)** | |

**INTRO**

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na kipindi cha tatu cha mchezo wetu mpya wa redio kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajipata pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Viongozi wa hapo kambini Talib na Chika wamezijumuisha jamii hizo mbili mahasimu kujadili katika makundi lakini Chika anatatizika na hatua ya Mulogo kumzungumzia maswala ya mapenzi. Jiunge nasi sasa, wakati ambapo mkewe Chifu Kipko anapoeleza kwamba hali ya mambo haitawahi kurudi kama awali lakini Chika anampa matumaini.

**Episode THREE: <u>“Women Have Their Say.”</u>**

1. **<u>MUSIC UP</u>**

**Scene 1**

**2.SFX Day time ambience (inside / late afternoon)**

**3.MOTHER:** Mimi ni mkewe Chifu Kipko na ni mama wa watoto watatu wa kiume. Wawili wao, Isingoma na Kato, ni mapacha. Vita vilizuka wilayani kwenye miezi sita iliyopita. Mume wangu na mtoto wangu wa kwanza, Jamal, walikimbilia mafichoni. Kato, pacha mwenzake Isi, alitoweka eneo fulani mwituni. Mimi na Isi tukakimbia kutoka kijijini peke yetu. Tuliletwa hapa kwenye kambi ya Dovani. Kambi yenyewe inasimamiwa na shirika la kiafrika lisilokuwa la kiserikali liitwalo *Saidia Afrika*. Shirika hili limekuwa likitusaidia kuanza maisha mapya hapa. Ni wazi kwamba maisha nyumbani kwetu hayatawahi kurejea hali yake ya zamani. Aaa! Mume wangu, sijui lililomsibu! Naomba isiwe kwamba yeye na watoto wetu walikamatwa na waasi.

## Scene 2

**4.SFX Footsteps approaching. Knocking on door, then opening**

**5.CHIKA:** Hodi! Hodi hapa! Shikamoo mama! Unafanya nini peke yako kwenye nyumba yenye giza?

**6.MOTHER:** aah! Marahaba Chika. **(big sigh)** Nilikuwa nikiifikiria familia yangu na vitu vyote tulivyopoteza.

**7.CHIKA:** Pole mama. **(Coming closer)** Wanaume hurudi tena vita vikimalizika. Tunapaswa kuweka matumaini kwamba walifanikiwa kujiunga na kambi nyingine ya wakimbizi.

**8.MOTHER:** Na vipi kuhusu makazi yetu na ardhi? Hakuna hata mmoja miongoni mwetu atakayepata chochote wakati tutakaporejea makwetu. Tunasikia kwamba majeshi ya serikali na yale ya waasi yalichoma misitu na mimea yetu ya mazao.

**9.CHIKA:** Najua. Lakini ..tuangazie upande mwingine na tuchukulie kwamba hali hiyo ni mwanzo mpya. Niliwahi kuishi katika eneo la Abanto na nakumbuka wilaya za Banega na Abanto zilitatizika sana kwa uharibifu wa misitu na pia watu walipigania ardhi ya malisho.

**10.MOTHER:** Hayo ni kweli. Mume wangu alijitahidi sana kuendeleza sera ya kufyeka ardhi. Hakuzingatia maoni ya Chifu Apaloo. Lakini alikuwa ameahidi kwamba jamii ingepata kazi mpya na pia mali.

**11.CHIKA:** Ndiyo. Hayo yameshapita. Tuna fursa nzuri sana sasa katika kambi ya Dovani kushirikiana kutafuta njia za kuzijenga upya jamii zetu.

**12.MOTHER: (Sigh)** Ardhi itakuwa imekwisha.

**13.CHIKA:** Inaweza kurudi hali yake ya zamani. Ndio sababu tuko hapa- kutafuta suluhisho... Toka nje mama upumzike kwenye kivuli cha mkuyu. Raha sana kuwa kwenye kivuli hicho.

**14.MOTHER:** Sawa. Asante Chika.

**15.CHIKA:** Tutaonana baadaye kwenye mkutano wa kamati ya kina mama kuhusu misitu. Tazama kule! Mwanao Isi yuko huko milimani pamoja na Akiki.

**16.MOTHER: (Laughing softly)** Alaa, ndiye yule! Nashukuru Mngu kuwa na Isi. Nilitamani siku zote kupata binti! Nashukuru kwamba huyo msichana mdogo tunakaa naye. Hadi familia yake itakapopatikana.

**<u>17.MUSIC UP</u>**

**Scene 3**

**18.SFX: Field - Sound of cows mooing and eating**

**19.AKIKI: (talking softly)** Sshh. Njoo! Acha nipande mgongoni mwako. Una pembe nzuri za kupendeza. Njoo!

**20.ISI: (gently)** Je Akiki unampenda ng'ombe wako mpya?

**21.AKIKI:** Kweli Isi. Ni wangu kweli?

**22.ISI:** Naam – ng'ombe wetu alizaa ndama wawili. Ni desturi yetu kuwapa jamaa zetu zawadi. Na wewe sasa ni dadangu mdogo! Huyu ng'ombe anakupenda! Umepanga kumpa jina gani?

**23.AKIKI:** Kiroko, kwa sababu ana madoa meupe usoni mwake!

**24.ISI: (laughing)** Vizuri Akiki! Kiroko! Jina zuri hilo. Ni ng'ombe wa thamani wa jamii ya wanyankole. Angalia pembe zake. Ng'ombe aina hii hawapatikani sana siku hizi.

**25.AKIKI:** Kwa nini?

**26.ISI:** Hawatoi maziwa mengi kama aina mpya ya ng'ombe. Aidha, ng'ombe wetu wa kiafrika hupenda kuzunguka na kulisha maeneo ya mbali. Hili ni tatizo kwa kweli.

**27.AKIKI:** Mbona liwe tatizo?

**28.ISI:** Kwa mfano, babangu alianza kufyeka majani katika ardhi yetu ili apande mimea zaidi ya mazao ya kuuza. Kwa hivyo ng'ombe wetu wakaanza kuzunguka katika eneo la Abanto wakitafuta malisho. Jamaa zake Chifu Apaloo walikasirishwa na jambo hilo. .

**29.AKIKI:** Kwa nini? Mtu anaweza kukasirishwa na ng'ombe?

**30.ISI: (laughing)** Walitukasirikia sisi, wala si ng'ombe, kwasababu tulikuwa tukiwalisha katika maeneo yao yenye malisho. Wanahitaji nyasi nyingi. Unadhani ng'ombe wao wangekula nini?

**31.AKIKI:** Mbona msiwalishe ng'ombe wenu pamoja? Wafaidike na mazao yenu, na nyinyi mfaidike na nyasi yao?

**32.ISI:** Alaa! Akiki – Tukuite mwanauchumi! Unalosema ni sawa lakini hatukuzingatia hayo. Ilikuwa habari ya "sisi na wao". Pengine sasa hivi tutashirikiana vyema zaidi hapa. Tazama- yule Talib pale...Anazungumza na Chifu Apalooo. Wanaonekana wadogo sana kutoka huku juu tuliko! Sijui wanazungumzia nini!

## Scene 4

**33. SFX Day sounds outside**

**34.CHIEF APALOO:** Talib nilisoma jambo la kushangaza kwenye maktaba ya afisi yenu.

**35.TALIB:** Nafurahi kusikia kwamba unatumia maktaba yetu Chifu Apaloo. Ehee! Uligundua nini?

**36.CHIEF APALOO:** Naam- unajua kwamba jamii moja ya vijijini kama vile Abanto hukata kuni kiasi mizigo mia tatu inayobebwa na punda... kwa mwezi? Si ajabu misitu yetu inakwisha hivyo kwa kasi. Tunaikatakata na kuichoma kwa tamaa ya fedha tunazopata. Na pesa zenyewe hata si nyingi hivyo. Wala si chochote si lolote tukilinganisha na madhara tunayosababisha.

**37.TALIB:** Unajua, mwanao anataka ufumbuzi wa kileo- nguvu za umeme kwa mfano, ili tupunguze matumizi ya kuni.

**38.CHIEF APALOO:** Aaakh! Mwanangu anadhamiria tu kujihusisha na biashara kubwa kubwa ili awe na nguvu katika jamii. Anafikiri ndio njia ya pekee ya kutajirika upesi.

**39.TALIB:** Labda. Lakini kuna watu wengi wengine wanaodai kwamba mabwawa na hifadhi za maji ndo mwelekeo wa siku za usoni. Inatakikana kutathmini mambo hayo na kufahamu faida na hasara zake kama tunataka kupata ufumbuzi wa kienyeji wa hayo mambo..

**40.CHIEF APALOO:** Naam! Nawajua jamaa zangu wa Abanto. Tunatakikana kuzingatia mambo ya msingi, tuelewe hali ya udongo, tufahamu umuhimu wa miti na pia misitu. Tunatakiwa kuhuisha tena misitu. Tupande mbegu zitakazoilisha dunia na kutulisha sisi pia.

**41.TALIB:** Looo! Chifu wewe ni mshairi ati!

**42.CHIEF APALOO:** Na kama mwanasayansi! Talib! Ninaandaa kitu ambacho natumai utakipenda!

**43.TALIB:** Alaa ? Ni nini?

**44.CHIEF: (Laughs)** Tulia! Bado ninaendelea kufanya utafiti lakini nitakujulisha wewe mwanzo pindi nitakapomaliza! Na kisha niwapelekea wanakamati wa kamati ya kina mama wanipe maoni yao! Ninajihisi kuwa na mchecheto! Huenda tukapata suluhu.

**<u>45.MUSIC UP</u>**

**Scene 5**

**46. SFX By water pump - Sound of water, washing and singing.**

**47.MULOGO:** Boo!

**48.CHIKA:** Ai! Sabuni imeniingia machoni. Nani wewe? Talib?

**49.MULOGO: (changing his voice to very deep)** Hapana siye! Ni mimi!

**50.CHIKA:** Mimi ndiye nani? Talib, ni wewe?

**51.MULOGO: (still very low voice)** Achana na hayo! Usinifanye nione wivu. Mimi ndiye mwanamume!

**52.CHIKA:** Aaakh…macho yangu yanawasha! Akh! Mulogo! Kumbe ni wewe! Macho yangu sasa yote ni mekundu!

**53.MULOGO: (normal voice but very flirty)** Hapana nawe! Si hayo macho meusi mazuri. Usiseme nimeuharibu urembo wako huo!

**54.CHIKA:** Unataka nini Mulogo? Si uungwana kumsumbua mwanamke anapooga. Ninahitaji faragha.

**55.MULOGO:** Ndio, bibi. Lakini mimi pia ninahitaji kuwa faragha nawe. Si kila siku mikutano na mijadala hii ya umma. Hatuwezi kupata muda wa faragha- mimi na wewe?

**56.CHIKA:** Hapa nimekuja kufanya kazi. Siwezi kuchanganya kazi na starehe.

**57.MULOGO:** Alaa! Kwa hivyo sina maana kwako eeh! Nilijuwa tu!

**58.CHIKA:** Aaah Mulogo! Nenda zako. Niache!

**59.MULOGO: (Walking away)** Tunatoka wilaya moja. Ninajua unakoishi. Tutakaporudi Abanto nitakutembelea na tutakuwa na faragha. Ninakuahidi hivyo. Kwaheri kwa sasa, binti mrembo.

**<u>60.MUSIC UP</u>**

**<u>Scene 6</u>**

**<u>61. SFX Day time sounds</u>**

**62.MOTHER: (FADE IN)** Tulipanda maharagwe aina ya soya kwa sababu yana lishe bora na ndiyo yanayofaa kwenye udongo huu. Tunaweza kuuza maharagwe ya ziada. Sasa, sisi kina mama tunatakikana kuwa na usemi kuhusu jinsi ya kuutumia na kuuhifadhi msitu.

**63.CHIKA:** Naam, Mama... kwa kuwa sisi ndio tunaokwenda kutafuta kuni. Tunakwenda kuteka maji pia na vitu hivi havipatikani kwa urahisi siku hizi. Tunajiumiza si haba ili kupata vitu vya kimsingi.

**<u>64.Women's voices express approval</u>**

**65.MOTHER:** Tunatakikana kuanza na malengo ya kamati yetu, Ama waonaje, Chika?

**66.CHIKA:** Ndio, kwanza tunapaswa kufahamu hali ya kisheria ya msitu wetu. Maanake tujue nani anayemiliki nini... na tubainishe haki zetu.

**67.MOTHER:** Najua mume wangu, Chifu Kipko aliiuzia kampuni ya BigWood eneo la hekta elfu tatu. Serikali yetu inamilika tena kipande kikubwa cha mwitu huo. Kuna ardhi ambayo inamilikiwa na machifu wa jamii zetu, lakini ni ardhi kiasi gani?

**68.CHIKA:** Tukishajua, tunaweza kujadiliana na wenyewe kuhusu jinsi ya kuhifadhi misitu na ardhi za kilimo kwa matumizi na maisha yetu.

**69.MOTHER:** Tunataka vipato kutokana na vitu tunavyovikuza, lakini hakuna tena kwenda kukata kuni mwituni. Ni kama kuiba na mwishowe tutamaliza kila kitu tusipoacha mwenendo huo. Tunatakikana kuwa wakulima wala si waharibifu.

**70.<u>MUSIC UP</u>**

**<u>Scene 7</u>**

**<u>71. SFX: Field - Cows mooing and eating</u>**

**72.ISI:** Akiki kitendawili?; Mti unapoonguka mwituni na hakuna mtu aliye karibu, je mti huto hutoa sauti?

**73.AKIKI:** Mti unapoanguka hutoa sauti...naam...sauti kama ya ng'ombe anayekaribia kukata roho... **(makes a wailing sound)**

**74.ISI:** Na je ndugu yangu Kato akianguka na kisha aombe msaada kwa sauti akiwa mbali, nitamsikia?

**75.AKIKI: (softly)** Moyoni mwako pengine. Hapo ndipo walipo mamangu, babangu na Sesi wangu, Moyoni mwangu. Isi. Tafadhali uimbe tena ule wimbo. Labda watatusikia!

**76.<u>ISI and AKIKI hum song softly.</u>**

**<u>77. Music Up</u>**

**OUTRO.**

Na huo kwa leo ndio mwisho wa kipindi chetu cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* cha mchezo wa redio "Mti unapoanguka..." ulioandikwa na Romie Singh unaoshughulikia suala la uharibifu wa misitu.

Tumegundua kwamba jamii ya mashambani hutumia mizigo mia tatu ya kuni inayobebwa na punda... kila mwezi. Hivyo basi Chifu Apaloo amefurahi kwamba huenda akavumbua njia ya kupunguza matumizi ya kuni kwa asilimia 50.

Usikose kujiunga nasi kwenye kipindi kijacho cha nne.

Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

Kwaheri kwa sasa.

**END OF EPISODE 3**